# Thamani ya Lishe na Usalama wa Chakula wa Dagaa Waliosindikwa katika Masoko Mawili ya Samaki Jijini Dar es Salaam, Tanzania

*— Matokeo kutoka kwa Majadiliano ya Vikundi vya Wadau —*

*Dk. Lydia Gaspare na Livinus Renatus, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

## Matokeo muhimu

- Kuna tofauti kubwa kati ya mbinu za usindikaji katika masoko ya samaki ya Kunduchi na Ferry. Kunduchi huzalisha dagaa kwa ajili ya masoko ya mbali kwa kutumia mbinu za kuchemsha na kukaushia juani ili kuongeza muda wa kuhifadhi na kurahisisha usafifishaji. Ferry huzingatia kukaanga kwa ajili ya matumizi ya haraka katika jamii za jirani. Tofauti hizi huunda miundombinu na mbinu za udhibiti zinazopatikana katika kila soko.
- Mbinu za usindikaji huamuliwa zaidi na sababu za kiuchumi na sababu za kiutendaji. Kuchemsha kunahusishwa zaidi na usafi na thamani ya lishe, ingawa huhitaji uwekezaji mkubwa wa vifaa, nguvukazi na nishati, hivyo kuifanya kuwa kazi inayowahusisha zaidi wanaume. Kukaanga huhitaji mtaji mdogo, hufaa kwa shughuli ndogo za kila siku, na kuhakikisha mtiririko wa mapato ya kila siku. Kwa sababu hizo, imekuwa njia maarufu zaidi miongoni mwa wanawake Kunduchi. Hata hivyo, katika soko la Ferry wanawake hukosa fursa ya kukaanga kutokana na mfumo wa umiliki wa pamoja wa majiko unaozuia upatikanaji wa majiko hayo kwa wanawake na kuwafanya wanaume kukutawala katika shughuli hii.
- Mapendeleo ya walaji yanaongozwa zaidi na ladha, bei, na upatikanaji. Dagaa waliokaangwa ni maarufu kwa ladha na urahisi wa maandalizi yake kwa ajili ya matumizi, hasa Ferry. Dagaa waliochemshwa hupendelewa na walaji wanaojali afya. Hata hivyo, dagaa waliokaushwa huathiriwa na msimu wa mvua ambapo usafi na usalama wake hutiliwa shaka zaidi.
- Mtazamo wa lishe na usalama wa chakula hutofautiana kulingana na mbinu ya usindikaji. Dagaa waliochemshwa na kukaushwa juani huonekana kuwa na lishe bora zaidi na usafi mzuri kwa sababu uchakataji wake hupunguza athari za vimelea vya magonjwan na huusisha chumvi. Waliokaushwa moja kwa moja juani hudhaniwa kuwa na virutubisho vingi zaidi ingawa uwezekano wa kuchafuliwa iwapo hawashughulikiwi vizuri ni mkubwa. Waliokaangwa huonekana kama si salama kiafya kutokana na mafuta yanayotumiwa mara kwa mara jambo linaloweza kusababisha uchafuzi wa kikemikali. Katika mbinu zote, kuna hatari zinazohusiana na uchafuzi wa taka ngumu (mfano mchanga na vumbi), mabaki ya kikemikali, ukuaji wa vimele na vijidudu hasa katika mazingira yenye viwango duni vya usafi.
- Mabadiliko ya misimu huathiri shughuli za usindikaji katika wingi na usalama cha dagaa wanaosindikwa. Wakati wa mvua, samaki wengi huvuliwa hivyo kuongeza usindikaji. Ingawa mvua kubwa huathiri mbinu zinazohusisha kukausha kwa matumizi ya jua na kuongeza uwezekano wa uchafuzi wa dagaa. Katika msimu huu walaji hulalamika kuhusu harufu mbaya ya dagaa wanaokausha pamoja na kuoza kwake. Msimu wa kiangazi huwezesha kukaushwa vizuri lakini samaki hupatiokana kwa uchache jambo ambalao hupunguza kiasi cha uchakataji utokanao na kuchemsha na kuanika. Kukaanga huendelea mwaka mzima bila kuathiriwa san ana misimu ya uvuvi mkubwa na upatikanaji hafifu wa samaki.
- Matumizi ya nishati husababisha madhara ya mazingira na afya. Matumizi makubwa ni ya nishati ya kuni ambayo husababisha madhara ya afya ya upumuaji na athari zitokanazo na ukataji miti. Ingawa Ferry imeanza kutumia gesi kwa kukaanga, lakini inasemekana ni ghali. Kunduchi mabadiliko yenye mwelekeo wa matumizi ya gesi bado yapo kwenye hatua za awali. Ijapokuwa kukaushwa moja kwa moja juani haina madhara makubwa ya mazingira lakini huathiriwa na hali ya hewa.

- Tofauti za kijinsia zipo wazi. Wanawake Kunduchi hutawala mbinu ya ukaangaji lakini hukumbana na vikwazo katika kuiendea mbinu ya kuchemsha kwa sababu ya gharama kubwa za miundombinu ya uchemshaji, nguvukazi pamoja na mifumo ya taasisi isiyo rafiki kwao. Kunduchi ni mwanamke mmoja tu anayemiliki jiko la kuchemsha na chanja za kuanikia dagaa. Hata hivyo, huwaajili wanaume kuliendesha jiko hilo wakati wa uchakataji. Hali ni tofauti Ferry ambapo kukaanga hutawaliwa zaidi na wanaume kwa mfumo wa umiliki wa jiko usiorithishwa au kuhamishwa kwenda kwa mmiliki mwingine. Hali hii huzuia wanawake kupiga hatua kiuchumi na kiushiriki katika mbinu hii ya ukaangaji.
- Kanuni za udhibiti hutofautiana baina ya sehemu hizi mbili. Wakati Kunduchi haina usimamizi mkubwa rasmi, ambapo wachakataji hawahitaji kujisajili au kupata leseni ambapo njia pekee za udhibiti zilizopo ni sheria ndogondogo za soko na tozo za faini ambazo hutozwa kwa wanaofungasha dagaa kinyume na taratibu zilizopo. Katika soko la Ferry mifumo ya usimamizi na udhibiti ina muundo mzuri ambapo ina leseni za lazima kwa kila mwaka kwa wachakataji na ukaguzi wa usafi wa kila siku, lakini utekelezaji hauna mwendelezo mzuri. Utunzaji wa kumbukumbu bado sio jambo la kisheria katika masoko yote mawili.
- Usafi na miundombinu ni changamoto kubwa pande zote mbili. Upatikanaji wa maji safi, mahala maalumu kwa ajili ya uchakataji na maeneo maalumu kwa kuhifadhia bidhaa ikishachakatwa bado ni changamoto. Wakati baadhi ya wasindikaji wanazingatia mbinu bora, kama vile matumizi ya glavu na usafi wa mara kwa mara, wengi wao hufanya kazi katika mazingira duni na ya muda ambayo yanahatarisha usafi wa chakula. Ingawa wasindikaji wengi wanatambua hatari hizi, wanakosa uwezo wa kifedha au msaada wa kitaasisi wa kuzikabili.
- Katika masoko yote mawili, kuna hitaji kubwa lililoelezwa wazi la msaada mahsusi. Wasindikaji wanaomba mafunzo ya kiufundi, upatikanaji wa vifaa, na miundombinu iliyoboreshwa. Wanawake, hususan, wanasisitiza umuhimu wa huduma za mikopo, taratibu za leseni zenye usawa, na upatikanaji wa teknolojia za kisasa kama vile vikausha vya jua. Pia kuna matarajio dhahiri ya ushiriki mkubwa zaidi kutoka kwa mashirika ya serikali na asasi za kiraia.
- Kwa kuzingatia changamoto hizi, kuna mapendekezo madhubuti yanayoweza kutekelezwa. Uwekezaji katika miundombinu unahitajika kwa haraka ili kuboresha upatikanaji wa maji safi, vikausha samaki, na mabanda ya usindikaji. Mbinu mbadala za nishati safi, kama vile gesi yenye ruzuku, zinapaswa kuhamasishwa, hasa katika eneo la Kunduchi, ili kupunguza athari za kimazingira na kiafya. Sera kuhusu umiliki wa majiko katika Ferry zinapaswa kufanyiwa marekebisho ili kuwezesha ushiriki kamili wa wanawake, ikijumuisha uwezo wa kurithi na kuhamisha umiliki.
- Mazingira ya udhibiti katika Kunduchi yanapaswa kuimarishwa kupitia masharti ya utoaji leseni, ukaguzi wa mara kwa mara, na matumizi ya taratibu zilizosanifiwa za utunzaji wa kumbukumbu. Kampeni za uhamasishaji kwa walaji zinapaswa kuangazia hatari za matumizi ya mafuta yaliyotumiwa zaidi ya mara moja na faida za kiafya zinazotokana na usindikaji salama.

